# K.C.P.E BOOSTER

## DARASA LA NANE MUHULA WA TATU - 2014

## KISWAHILI: LUGHA

SOMA MAAGIZO YAFUATAYO

1. Tumia penseli ya kawaida.
2. Hakikisha ya kwamba yafuatayo umeandika katika karatasi ya majibu:

Muda: Saa 1 Dak. 40

I) JINA LAKO II) JINA LA SHULE YAKO III) NAMBARI YA MTIHANI

***Soma vifungu vifuatavyo, vina maswali 1 hadi 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Nidhamu au __1__ ni jambo __2__ na hususan kwa mwanafunzi ambaye __3__ kuendelea mbele na masomo yake. __4__ na __5__ wa siku hizi wameingiwa na kasumba ya wazungu kutokana na yale wanayoona kwenye __6__ na kusikiliza kwenye redio. Wanafunzi wote wakumbuke kuwa mwacha __7__ ni mtumwa.

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| 1. | azima | taadhimu | taadhima | azimia |
| 2. | asusi | hasidi | asisi | azizi |
| 3. | anaazimu | anawaziana | anaazimia | azimisha |
| 4. | banati | binamiti | binti | benati |
| 5. | mabwana | shababi | mabibi | mabwega |
| 6. | hewa | aidha | ngamizi | matangazo |
| 7. | asali | asili | azili | nzimisho |

Usirudi kabla hujatembelea kusini __8__ Pwani. Utaabiri kivuko cha Likoni. Ukifika ng'ambo ya pili, utaanza kuona tamaduni __9__ Pwani. Nyumba zime __10__ kwa __11__ ya minazi. Huwezi kuona kufuli __12__ mlangoni kwani wote ni ndugu. Aidha utaona vyakula vya __13__. Wao ni __14__ wa mapishi. Wanajua __15__ aina mbalimbali za vyakula wakakuacha ukiramba vidole.

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| 8. | wa | ya | za | cha |
| 9. | za | ya | wa | la |
| 10. | ezua | kuandikwa | ezekwa | kuandikwa |
| 11. | mabali | miti | makuti | madafu |
| 12. | lolote | yoyote | zozote | chochote |
| 13. | kuazili | kiasili | kienyechi | viasili |
| 14. | galacha | walegevu | magaidi | mabozi |
| 15. | kukaranga | kukaanga | kuchemsha | kutokosa |

***Kutoka swali 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.***

16. Andika wingi wa sentensi ifuatayo.
    Mweledi alikunywa uji kisha akatapika.
    A. Waeledi walikunywa nyuji kisha wakatapika.
    B. Waledi walikunywa uji kisha wakatapika.
    C. Waulidi walikunywa nyuji kisha wakatapika.
    D. Waledi walikunywa uji kisha akatapika.
17. Chagua kiashiria katika sentensi hii:
    Dukani pake ndipo alipomwona mgeni yule.
    A. pake B. yule
    C. alipomwona D. mgeni
18. Nomino kiumbe iko katika ngeli gani?
    A. KI - VI B. A - WA
    C. I - ZI D. KU - KU
19. Chagua methali iliyo na mshabaha na:
    Mnyonyore haunukii hupendeza mauaye.
    A. Kula kutamu kulima mavune
    B. Usione wembamba wa reli, gari moshi hupita
    C. Mchagua samaki hupata aliyechina
    D; Chema chajiuza kibaya chajitembeza

20. Mtu anapopatwa na msiba hupatiwa mkono wa
A. yamini B. tanzia
C. tahania D.shemali

21. Chagua nomino iliyoambatanishwa sahihi na amali yake.
A. Mrumba - mtu anayewawinda wanyama
B. Dalali - anayetafsiri lugha
C. Mutribu - anayeghani mashairi
D. Gawadi - anayepeleka habari ya posa

22. Ujumbe unaotumiwa kwa kutumia tarakilishi na ambayo ni njia haraka sana ya mawasiliano huitwa ________
A. utandawazi
B. kipepesi
C. arafa
D. barua meme

23. Ni sentensi ipi inayoonyesha ji ya hali?
A. Jitu hili lilitisha
B. Anajisemea mwenyewe
C. Uogeleaji ulituvutia
D. Ana jasho jingi

24. Onyesha msemo unaoashiria maana ya kuvumilia uchungu.
A. Kuvaa mchi na kujitanda kuni
B. Kuvuka kilemba cha ukoka
C. Kujipalia makaa
D. Kumeza mrututu

25. Nyoka mwenye sumu si mwengine yeyote ila bafe. Maneno yaliyopigwa mistari yanaashiria nini?
A. Viashiria visisitizi
B. Vivumishi halisi
C. Vivumishi ashiria
D. Viwakilishi

26. Shairi ambalo limegawanywa katika vipande viwili huitwa ________
A. manthawi
B. ukwafi
C. manthami
D. ukwapi

27. Teaua kiunganishi sahihi.
Moraa alipokwenda cheteni alinunua bidhaa tele ________ mboga. Viazi vitamu, viungo vya upishi na matunda.
A. aghalabu
B. mighairi ya
C. sembuse
D. mathalani

28. Pindo au kona ya barabara ni ________
A. duara
B. kuruba
C. ghorofa
D. ghubari

29. Pesa anazo tumia mtu ili kuanzisha biashara zinajulikana kama ________
A. mtaji
B. arbuni
C. karadha
D. fidia

30. Ni sayiri ipi ambayo ni ndogo kuliko zote zinazojulikana?
A. Zuhura
B. Utaridi
C. Zebaki
D. Sarteni

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata 31 - 40.***

Siasa ni nini? Siasa ni itikadi inayofuatwa na nchi, kundi au jamii fulani ambayo ni msingi wa kuendesha uchumi, utamaduni na mwenendo mzima wa maisha ya nchi au jaii hiyo.

Wakenya wengi wamepotoka na kufikiria kuw siasa ni kufurahia vya bwerere kila baada ya miaka mitano uchaguzi mkuu unapotangazwa. Hawajui kwamba siasa i utaratibu mkuu mwafaka wa kutenda hususan mambo ya utawala kwa haki na maadili yafaayo. Siasa bora chambilecho rais wetu, ni maisha bora. Wakenya wakifuata siasa zilizokomaa bila shaka tutafurahia matunda yake.

Matunda matamu ya siasa ni kama vile uimarishaji wa elimu, shughuli za afya, barabara nzuri, usalama na hali ya utulivu katika nchi. Kinyume ni cha haya, siasa mbaya huzusha uhasama. Umaskini na mchafuko wa maisha kwa jumla. Kwa Wakenya, hasa tunapokaribia uchaguzi mkuu swali kuu ni hili, je tutawachagua viongozi wenye vipawa vya uongozi walielekeza jahazi letu fanakani au tutahongwa na kuchagua mabwenyenye wafisadi watakaolizamisha jahazi letu?

Haki ya mwananchi katika siasa za nchi yake ni ipi? Bila shaka ni kutumia kura yake kumchagua mwakilishi anayefaa ili kusaidia kutunga sheria nzuri bungeni zitakazoongoza shughuli za kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa manufaa ya Wakenya.

Jambo jingine muhimu wakati wa kampeni za uchaguzi ujao ni kudumisha amani na kutofuata viongozi wa vyama mbalimbali vya kisiasa. Watakaoibuka washindi wayashughulikie maslahi ya wananchi kabla ya mahitaji yao binafsi.

---

31. Wananchi yafaa washiriki katika siasa za nchi yao ________
   A. kuwachagua viongozi
   B. kujikumbusha wakati wa uchaguzi
   C. kuwachagua mabwenyenye kuongoza jahazi
   D. kuwachagua viongozi wafaao

32. Wananchi wanaharibu siasa za nchi kwa ________
   A. kujiunga na vyama vya kisiasa
   B. kutawala bila haki
   C. kukubali kuhongwa na wagombea uchaguzi
   D. kutunga sheria zisizofaa

33. Kati ya mambo haya ni lipi lisilo tunda la siasa bora?
   A. Siha bora
   B. Ukarabati wa barabara
   C. Rangaito
   D. Maisha na maendeleo kwa wananchi

34. Jahazi lililotajwa katika ufahamu ni ________
   A. meli
   B. wafisadi
   C. vipawa vya uongozi
   D. maisha na maendeleo kwa wananchi

35. Neno komaa limetumiwa katika habari hii kwa maana ya ________
   A. kuimarika na kufika kiwango cha juu
   B. kufika mwisho
   C. anzishwa
   D. fumbuliwa

36. Neno hongo halina maana sawa na ________
   A. chirimiri
   B. ufisadi
   C. rushwa
   D. kadhongo

37. Mwakilishi wa wananchi katika serikali za mitaa huitwa ________
   A. mbuge
   B. diwani
   C. balozi
   D. chifu

38. Wawakilishi wengine wa wananchi huwakosea sana kwa ________
   A. kukosa kipawa
   B. kupokea hongo
   C. kupinga maendeleo
   D. kuyaweka maslahi yao

39. Chagua sentensi sahihi kulingana na habari uliyosoma.
   A. Vyama vingi vya kisiasa havifai
   B. Siasa bora huleta ustawi nchini
   C. Mabwenyenye pekee ndio wafaao bungeni
   D. Matunda ya siasa ni uhasama

40. Kichwa kinachofaa zaidi kwa habari hii ni ________
   A. Siasa bora
   B. Vyama vingi vya kisiasa
   C. Uchaguzi mwakani
   D. Amani na upendo

---

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 - 50.***

Bingi Lulu alikuwa hurulaini. Fauka ya hayo, alilelewa vyema kwa maadili maridhawa yaliyompendeza na kumfurahisha kila adinasi. Aidha alitunukiwa akili pevu na tambuzi iliyomwezesha kusoma hadi chuo kikuu na kupata shahada ya uzamifu.

Alitaalamika katika taaluma ya uhasibu akiwa na umri mdogo sana ukilinganishwa na wenzake wenye kiwango hicho cha elimu.

Pindi alipohitimu masomo yake, aliajiriwa kazi na shirika moja lisilo la kiserikali kwa mshahara wa

donge nono. Urembo wake, elimu na kitita cha pesa vilifanya wanaume wengi kumkaramia mithili ya kinamasi jangwani wakiwa na lengo la kumchumbia. Maadamu Lulu hangeweza kukashifu maumbile akasalimu amri. Alimwenzi mvuli mmoja ambaye alikuwa akifanya naye ingawa katika idara tofauti.

Usuhuba wao ulijengeka na kuwa na chanda na pete. Wakaona kwamba njia ya pekee ya kufurahia upeo huu wa mapenzi ni kufunga pingu za maisha. Mshenga alipatikana na kuwaarifu wazazi wa wachumba kuhusu nia yao ya kufunga ndoa. Wazazi nao kutoka pande zote wakakubali bila ya pingamizi zozote. Juhudi za mshenga zikawakutanisha wavyele wa wachumba, mahari yakajadiliwa na kulipwa na hatimaye mikakati kabambe ya harusi ikaanza na kushika kasi. Tabasamu zikajaa nyusoni pa wachumba.

Waliosema kwamba dunia ni duara, huzunguka kama pia, waligonga ndipo. Siku moja mama Lulu alimkuta akilia kwikwikwi na kupiga kite, alipmdadisi, aliyoyasikia yalimwatua moyo. Lulu alimweleza mamaye kwamba mpenzi wake Tema, alimtaliki na kumchukuwa msichana mwingine. Tema aliona kwamba Lulu hampendi, kwa kutaka wangojee urasimu wa ndoa ambao ingechukua muda.

Mamaye Lulu alimliwaza na kumfariji akamshauri amsahau mwanaume asiyeheshimu mkataba. Kweli uchungu wa mwana aujuaye ni mzazi, Lulu alizingatia mashauri ya mama yake. Alihama akaenda kufanya kazi ya kuwahudumia watoto mayatima baada ya Tema kumtema Lulu alimwoa mpenzi mwengine. Hakumjulia Lulu la heri wala la shari.

Lulu aliendelea kuchapa kazi. Hatimaye huko alipata ghulamu mmoja mtanashati aliyempenda akamwamini na kumthamini. Walioana baada ya kujuana na kuchumbiana miaka mitatu wakaishi raha mustarehe. Yakini, Mola hamtupi mja wake.

---

41. "........... alikuwa hurulaini." Ni fani gani ya lugha iliyotumika hapa?
    A. Tashbihi B. Msemo
    C. Takriri D. Istiara
42. Lulu alikuwa banati wa aina gani?
    A. Wa kufuata rubaa
    B. Wa kufuata adili
    C. Wa kufuata msimamo wake
    D. Wa kufuata upepo
43. Tunu iliyotunukiwa Lulu ilitoka kwa nani?
    A. Wazazi B. Mola
    C. Walimu D. Marafiki
44. Msemo "akasalimu amri" imetumika katika taarifa. Maana yake kulingana na habari ni _____
    A. akakubali mapenzi
    B. akakataa mapenzi
    C. akatoroka
    D. akaamrisha
45. Mshenga hufanya kazi gani?
    A. Mtu anayevuruga ndoa
    B. Mtu anayechunga ndoa
    C. Ni sawa na mhenga
    D. Mtu anayetumwa kupeleka posa
46. ............. 'tabasmu zikajaa nyusoni pa wachumba.' Ni methali gani ambayo ingefaa zaidi kueleza maneno haya?
    A. Ajuaye kupendwa haachi kujisahau
    B. Mwenda pole hajikwai
    C. Mapenzi ni kipofu
    D. Kipendacho moyo ni dawa
47. Chagua sentensi ambayo si sahihi kulingana na taarifa uliyoisoma.
    A. Lulu alilia kwa sababu aliachwa na mchumba wake
    B. Tema alifariki baada ya miaka miwili walipoachana na Lulu
    C. Nasaha ambayo Lulu alipewa na mama yake ilimfaa
    D. Lulu aliwafariji na kuwaauni wasiobahatika jamii
48. Kulingana na taarifa, ni dhahiri shahiri kwamba Tema alikuwa kijana _________
    A. laghai B. gaidi
    C. mpwamu D. mwadilifu
49. Malipo ya kuolewa huitwa _________
    A. mapoza B. kiangazamacho
    C. mpwamu D. mahari
50. Kwa nini Lulu aliomba uhamisho?
    A. Ili aweze kumpata mchumba mwingine
    B. Ili aweze kuwahudumia mayatima wakongwe na wenye UKIMWI vizuri
    C. Ili atoke katika mazingira ya nyumbani
    D. Ili kughafilika mkasa uliompata